


Hadithi ya Peter Rabbit

Hadithi

ya

Peter Rabbit

Hapo zamani za kale kulikuwa na sungura wadogo wanne, na majina yao yalikuwa ni *Flopsy*, *Mopsy*, *Cotton-tail* na *Peter*.



Waliishi na mama yao porini kwenye eneo lenye udongo wa kichanga, mvunguni mwa mzizi ya mti mkubwa sana aina ya msonobari. Mama yao aliitwa Mama Rabbit. Baba yao alishakufa zamani.



“Haya sasa wapendwa,” alisema Mama Rabbit asubuhi moja “Mnaweza kwenda kucheza viungani

ama kule kando ya njia, ila tafadhali msiende kwenye
bustani ya Bwana McGregor, kwani
Marehemu Baba yenu alipata ajali kule; alibankwa
ndafu na Mama McGregor."



“Haya
nendeni
wanangu
ila mcheze
vizuri
msifanye
shari. Mimi
natoka
kidogo.”



Kisha Mama Rabbit akachukua kikapu na mwavuli wake na kupita kichochoroni chini ya miti kuelekea kwenye duka la mikate. Akanunua mkate mkubwa wa